# AFYA NA UPONYAJI WA KIUNGU



PASTOR JAMES KALEKWA

# AFYA NA UPONYAJI WA KIUNGU NI FUNGU LANGU!

**James Kalekwa**

## Yaliyomo kitabuni:

Salamu za Mama Mchungaji JK. ....................................................4

MAWAZO YA MUNGU. ..........6

TAFSIRI YA AFYA NA UPONYAJI WA KIUNGU....... 17

Kuhusu Afya: ........................... 17

Kuhusu Uponyaji/Tiba: ....... 30

NAMNA YA KUTEMBEA KWENYE AFYA YA KIUNGU. ..................................................39

Kuhusu Mwandishi: ................. 47

Kuhusu New Vine Church:..... 48

Mawasiliano na Mwandishi: .. 49

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025
Dodoma, Tanzania

## MAWAZO YA MUNGU.

Yeremia 29:11

*Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.*

Andiko hili linaonyesha kuwa kinachozungumza hapa ni mawazo ya Mungu mwenyewe kumuelekea mwanadamu. Na kutokea kwenye wazo kuu la andiko kuna mambo matano ya kujifunza/kuyatazama kuhusiana na mawazo ya Mungu.

1. **Mungu anakuwazia.** Kila mwanadamu, ki mahususi wewe upo kwenye mawazo ya Mungu. Hivi unajua Mungu ana mambo mengi sana ya kufanya. Kiasi kwamba ingekuwa ni sawa tu akiendelea bila kumuwazia yeyote kati yetu. Ndiyo maana wanaomuelewa Mungu na ukuu wake walifika mahali pa kuitika kwa kusema, Zaburi 8:4, "*Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie?*"

   Hili lilikuwa ni neno la kutia moyo sana kwa taifa la Israeli ya kwamba Mungu anawawazia. Huyu Mungu hajabadilika,

hata sasa anakuwazia… ananiwazia! Hiyo ibaki kuwa kweli ndani ya moyo wako.

Hata hivyo, ningependa uone kwenye tafsiri zingine za Biblia ya lugha ya Kiswahili (Tafsiri ya Biblia Habari Njema – BHN na tafsiri ya NENO). Kile ambacho ungedhani ni mawazo tu, kimepewa jina ambalo litaeleweka kwa urahisi kwako.

BHN, *"Maana, mimi Mwenyezi-Mungu ninajua mambo niliyowapangia. Nimewapangieni mema na si mabaya, ili mpate kuwa na tumaini la baadaye."*

NENO, *“Kwa maana ninajua mipango niliyo nayo kwa ajili yenu,” asema Bwana, “ni mipango ya kuwafanikisha na wala si ya kuwadhuru, ni mipango ya kuwapa tumaini katika siku zijazo.”*

- Mambo niliyowapangia
- Mipango niliyo nayo kwa ajili yenu

Lengo la kufanya rejea kwenye tafsiri nyinginezo ni ili kuelewa kwa mapana ha kina ni jambo gani hasa linawasilishwa hapa. Kumbe si mawazo tu yanayokuja na kuondoka… Kumbe, ni mipango; mambo yaliyo kwenye mtiririko na uelekeo maalum. Kumbe si mambo ya kubahatisha

tu. Mungu ana mipango na maisha ya watu wake.

Huwa ninaelewa hivi, ya kwamba Mungu hakuniumba kisha akaanza kushangaa au kujiuliza kwa nini aliniumba. Kilichompelekea kuniumba ni mpango wake kwangu. Mungu hajatuleta wenye haya maisha bila uwepo wa mpango wake maisha yanafaa kuwaje.

Iruhusu hiyo kweli iingie na kutulia ndani ya moyo wako!

2. **Mawazo ya Mungu kwa ajili yako ni mawazo ya Amani na tumaini**. Mungu

hajawahi kukuwazia wala hana mpango wa kukuwazia mabaya. Kwa mujibu wa neno lake anakuazia mambo ya Amani na mambo ya tumaini kwenye maisha yako. Kwa kuwa hapo awali tulichagua kuona kutoka kwenye tafsiri nyingine ya kwamba kumbe si mawazo tu bali ni mipango au mambo anayopanga kwa ajili yetu.

Mipango ya Mungu ni ya amani na tumaini. Yaani, hapa kinachomaanishwa ni kwamba yaliyomo *"contents"* kwenye kitabu cha mipango ya Mungu ni amani na tumaini. Na hata kama kwa mwonekano wan je,

yatakuwa ya kawaida au hayafurahishi, basi uwe na uhakika hatimaye ni mema na amani! Ni salama pia kitheolojia kutafsiri ya kwamba si tu yaliyomo *"contents"* bali hata njia za kuyatekeleza yaliyomo ni njia za amani! Unakumbuka namna ambavyo Yusufu mwana wa Yakobo anavyoyaeleza mawazo ya Mungu baada ya kujifunua kwa nduguze?

Mwanzo 50:20 (NENO), *"Mlikusudia kunidhuru,* ***lakini Mungu alikusudia mema,*** *ili litimie hili linalofanyika sasa, kuokoa maisha ya watu wengi."*

*Mwanzo 50:20 (SUV) "Nanyi kweli mlinikusudia mabaya,* ***bali Mungu aliyakusudia kuwa mema,*** *ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo."*

Ni rahisi kusherehekea sentensi hiyo ikiwa tu hujui njia aliyoipitia Yusufu. Anaonyesha wazi ya kuwa njia hiyo ilikusudiwa/iliwaziwa/iliwekewa mipango na wanadamu ya kumdhuru na kumletea mabaya. Hata hivyo, hitimisho lake linalotokana na uelewa wake juu ya mipango ya Mungu ni kwamba kulikuwa na mema katika njia hiyo; au ni sawa pia kudhani kuwa Mungu

aliikomboa njia hiyo na kuyageuza mabaya yote yatumike kuleta mema.

Vyovyote vile, hitimisho ni kwamba mawazo ya Mungu kwa ajili ya watu wake ni ya amani na tumaini!
Iruhusu hiyo kweli iingie na kutulia ndani ya moyo wako!

3. **Mema yako mbele yako!** Kwa kadiri siku zako za maisha zinavyoendelea mbele, ndivyo unavyozidi kuona/kusogelea mema na amani kwenye maisha yako. Kwenye utaratibu wa Mungu kwa kadiri unavyoenda

mbele ndivyo unavyozidi kuona wema, Amani na uzuri wa Mungu kwenye maisha yako. Kila leo yako ni nzuri kuliko jana yako.

Mit 4:18 (SUV), *“Bali njia ya wenye haki* ***ni kama nuru ing’aayo, Ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu.****”*

4. **Hatimaye utakuwa na mwisho mwema na wa Amani**. Kwenye haya maisha hupaswi kutarajia mabaya kwenye kesho yako kwa sababu kwa mujibu wa neno la Mungu kesho yako imehakikishwa kuwa yenye wema na Amani.

Tamati ya mambo yote ni Mungu kukupa utukufu au mwisho mwema!

5. Mojawapo ya mambo mema na ya Amani ambayo Mungu anakuwazia ni eneo la **afya na uponyaji**. Maadamu Mungu anatuwazia kuhusiana na Afya na uponyaji, basi ni vizuri tukijua anawazaje kutokea kwenye neno lake.

Ni jambo moja kufahamu ya kwamba Mungu anakuwazia mambo mema; ana mipango mizuri kukuhusu. Ni jambo la tofauti kabisa kufahamu hayo mema; hiyo mipango ni ipi hasa. Tena kwenye kila nyanja ya maisha. Mungu anawaza nini kuhusu afya yangu?

# TAFSIRI YA AFYA NA UPONYAJI WA KIUNGU.

## Kuhusu Afya:

Kutokea hapa tupate tafsiri kadhaa za Afya ya kiungu. Mtu hutambuliwa kuwa na afya pala anapokuwa:

- ✓ Katika hali nzuri mbali na magonjwa kimwili, kiakili, kijamii na kiroho.
- ✓ ni hali ya kuwa na hali ya utimamu wa mwili, akili na roho kwa endelevu.
- ✓ Ni kuwa na kingamwili dhidi ya changamoto za kiafya; kingamwili zipo kuzuia magonjwa yasiingie.
- ✓ Ni kuitunza uzima ulio nao usishambuliwe na magonjwa kwa

mtindo wa maisha – kama chakula na mazoezi.

Kitabibu, inafahamika na kukubalika kabisa ya kwamba mtu anaweza kuwa na afya na anapaswa kuwa nayo; na afya inayozungumzwa ni inayoenda na tafsiri ulizozisoma hapo awali.

Yaani kuwa na afya si ajabu… inawezekana na inatakiwa kuwa hivyo kitabibu.

Umewahi kuwaona watu wanashhughulika na mtindo wao wa maisha kama vile namna yao ulaji na mazoezi ya mwili? Lengo lao huwa ni kufikia mahali pa afya njema! Ninachokisema ni hiki, afya ni lengo

linalofikika kibinadamu kabisa na hata si kunai makuu au kujenga kasri hewani.

Kama lengo la afya linaweza kufikika, je hudhani ya kwamba Mungu anayo mawazo/mpango kwenye neno lake kuhisiana na afya za miili, akili na roho zetu? Hufikiri kuna namna ya kiungu ya kuwa na afya?

Baada ya kushuhudia hali za magonjwa kwa watu niwapendao na kwa sehemu kwenye maisha yangu binafsi, nilifikia mahai pa kujihoji maswali haya. Kama Mungu amekusudia watu wale aina fulani ya vyakula na wawe na mtindo fulani wa

kimaisha ili wawe na afya njema – jambo ambalo ninakubaliana nalo kwa asilimia zote kabisa.

1 Tim 4:8 (SUV), *"Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye."*

Baada ya kutafiti kwenye neno la Mungu, na kujifunza kisha kusikia shuhuda za watu kadhaa wa Mungu, nilifkia kwenye hitimisho ya kwamba iko namna ya kiungu inayohusiana na afya yangu… yapo mawazo ya Mungu… upo mpango wa Mungu kuhusiana na afya yangu!

Kwa hiyo basi, kuna afya kwa namna ya kitabibu na kuna afya kwa namna ya kiungu. Unielewe vizuri hapa… sisemi ya kwamba njia za kitabibu ni za kishetani au hazitokani na Mungu. Bali ninatumia maneno haya nikimaanisha kuna kanuni ambazo ni za kiroho na zinatekelezwa kiroho ili kufikia mahala pa afya ya kiungu. Wakati huo huo ninakubaliana na ukweli ya kwamba kila maarifa sahihi nay a kweli ya kitabibu yanatokana na yanatoa kwa Mungu!

Kwa mfano, ni vyema ukafahamu ya kwamba kingamwili inatengenezwa, na ili uwe na afya ya kiungu ni lazima kinga

ijengwe kwa kula aina fulani ya neno la Mungu.

Hii ni kinga unayoipata kwa njia za kiroho/kwa msaada wa Mungu na si kwa njia za afya za kibinadamu zilizozoeleka.
Kutoka 23:25, "*Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; nami* ***nitakuondolea ugonjwa kati yako.****"*

Kuna uwezekano kabisa wa Mungu kuondoa magonjwa katikati yako, na jukumu lako ni kumtambua kama Mungu anayeweza kukuondolea hayo magonjwa kwa sababu tumeona hivyo kutokea kwenye neno lake.

Zaburi 91:10-12, “*Mabaya hayatakupata wewe,Wala tauni haitaikaribia hema yako.* ***Kwa kuwa atakuagizia malaika zake Wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua,*** *Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.”*

Kutoka 9:26, *Katika nchi ya Gosheni peke yake, waliokaaa wana wa Israeli, haikuwako mvua ya mawe.*

Umgundua kwenye hayo Maandiko niliyoyarejelea hapo awali kuna namna watu wa Mungu wanawekwa mbali na magonjwa, tauni (magonjwa ya mlipuko) na madhira ya namna mbalimbali?

Umegundua hizo zinazotumika ni kanuni za kiungu zaidi kuwaweka watu katika hali ya afya – *kumtumikia Mungu, kuagiziwa huduma ya malaika, kukingwa!*

Hakuna tabibu atakuambia kuhusu kanuni hizo. Si kwamba ni watu wabaya lakini hazifahamiki kwenye ulimwengu wao. Hata hivyo, ile kwamba hazifahamika, haiondoi uhalali ya kwamba Mungu alizitumia kuhusiana na faya za watu wake.

Mungu mwenye kanuni ya kuwakinga watu wake dhidi ya mabaya, bado hata leo anaweza kukukinga dhidi ya kila aina ya ubaya na uharibifu.

Hebu tazama neno la Mungu linavyosema tena kuhusu kanuni hizi za kiafya kwa namna ya kiungu.

Zaburi 105:37, *Akawatoa hali wana fedha na dhahabu, katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa.*

Hili neno asiwepo *"mwenye kukwaa"* kwenye tafsiri nyingine husema *"no feeble amongst them!"*. Kuwa feeble ni kuwa mlegevu, dhaifu au mnyonge kwa sababu ya kukosa chakula au umri mkubwa.

Kumbuka hawa watu wazuri wa Mungu walikuwa kwenye safari ya jangwani kwa muda wa miaka arobaini (40) na hakukuwa na mtu mdhaifu miongoni mwao.

Mungu alifungulia kanuni ya afya ya kiungu itende kazi kwao.

Isaya 53:4-5

*Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya Amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona*.

Siku utakayochagua kumwamini Bwana kwa nguvu, ndiyo siku utakayopokea afya ya kiungu. Si sehemu ya uelekevu wa moyo na unyenyekevu kujivunia au kujiambatanisha na magonjwa na

madhaifu. Mpendwa wangu, magonjwa si jina mbadala… si kisawe (synonym) cha utakatifu!

Mungu hatarajii kutuona tukijivunia magonjwa na udhaifu kwa sababu amesha tuondolea na ameshatukinga dhidi yake kama alivyosema kwenye neno lake. Ushahidi mwingi unaonyesha Mungu alifanya hivyo na kwa sababu hiyo aweza kufanya hivyo kwa watu wake hata sasa.

Hebu tazama ushuhuda wa mzee wa miaka themanini sasa; ambaye aliyetembea jangwani kwa miaka arobaini. Anasimama hatimaye na kuelezea hali ya afya yake kama hoja ya msingi kwa nini apewe mlima

husika akapigane na kuwaondoshea mbali wanaoukalia ili auchukue kama urithi wake!

Yoshua 14:10-11, *"Sasa basi, angalia, yeye BWANA ameniweka hai, kama alivyosema, miaka hii arobaini na mitano, tangu wakati huo BWANA alipomwambia Musa neno hilo, wakati Israeli waliokuwa wakienenda barani; na sasa tazama, hivi leo nimepata miaka themanini na mitano umri wangu.* ***11Hata sasa mimi nina nguvu zangu hivi leo kama nilivyokuwa siku hiyo Musa aliyonituma; kama nguvu zangu zilivyokuwa wakati huo, na nguvu zangu ndivyo zilivyo sasa, kwa vita na kwa kutoka nje na kuingia ndani.****"*

Mzee anajisikia utimamu wa mwili. Mzee Kalebu mwana wa Yefune, anajisikia kama siku za ujana wake. Yuko tayari kwenda vitani. Ni siri gani imemtunza? Hakukuwa na mwenye kukwaa!

Huo ndiyo ushuhuda wako katika jina la Yesu Kristo. Kwa kadiri unavyoendelea kiumri, uwe imara na thabiti uweze kutimiliza kazi ya Mungu na makusudi aliyokuwekea mbele yako. Uweze kuchukua kila mlima na kupigana kila vita umiliki milki zako katika jina la Yesu Kristo!

## Kuhusu Uponyaji/Tiba:

Kwa ujumla wake uponyaji/Tiba:

- Ni ***afua*** ambayo hufanyika (intervention) kwenye changamoto ya kiafya inayoendelea ili kuleta suluhisho.
- Ni utendaji na utoaji wa tiba ili kuondokana na tatizo la kiafya lililokuwako.
- Afua hiyo iletayo tiba/uponyaji hufanyika kwa njia za kisayansi au tiba-mbadala zinazokubalika. Yaani, ni namna za kibinadamu.

Sasa, nimeyaunganisha maneno uponyaji na tiba kwa pamoja. Ninachokifanya hapa kuleta ulinganifu baina ya afya na

uponyaji/tiba. Ninamaanisha, afya ni kuzuia magonjwa yasiingie mwilini na uponyaji/tiba ni kufanya afua fulani ili kuondoa magonjwa yaliyoingia mwilini tayari.

Hata hivyo, tiba ni tendo la kitabibu na uponyaji ni tendo la kiungu. Kwa minajiri ya ulinganifu niliokuwa nikiufanya na fya, vyote vimeangukia kwenye daraja la fua zinalenga kuondoa ugonjwa. Hata hivyo, moja ni afua ya wanadamu ilhali nyingine ni ya Mungu mwenywe!

Sasa, ninataka nilete mkazo huu kwako. Kitabibu, inakubalika kabisa ya kwamba magonjwa, udhaifu au ulegevu wa kimwili

unaweza kuondolewa kabisa na hata usirudi tena kwa njia za kibinadamu. Ndiyo, tiba ina machaguo mengi na hapa nimezungumzia chaguo moja tu!

Kwa hiyo, wanadamu wanakubaliana na kweli ya kwamba magonjwa yanaweza kuitikia afua na kuondoka mwilini kabisa.

Kwa upande mwingine, uponyaji ni tendo la kiungu, kimiujiza na kwa namna ambayo haina maelezo ya kisayansi kibinadamu. Ile ya kwamba wanadamu hawawezi kuelezea kwa wakati huo haimaanishi si njia halali au halisia. Hiyo ni kuonyesha ukomo wa fikra za kibinadamu!

Kwa kuwa hoja ya msingi ni kwamba magonjwa yanaweza kuitikia afua na kuondoka, basi kuna namna ya kiungu ya kuyaondosha magonjwa yaliyoingia kwenye mwili wa mtu!

Uponyaji ni kwa ajili ya mtu ambaye kwa namna fulani afya yake imeshambuliwa, amepatwa na magonjwa, amepatwa na udhaifu, afya yake imeyumbishwa na adui.

Habari njema ni kwamba Mungu anayo njia na mawazo ya kukuponya na kukuondolea hayo magonjwa, kwa sababu amekusudia kukuponya.

Zaburi 107:20, "*Hulituma neno lake, huwaponya, huwatoa katika maangamizo yao.*"

Mungu anapolituma neno, haliji kutalii bali linakuja kwa kusudi. Na kususdi mojawapo ni kwa ajili ya kukuponya.

Mathayo 4:23, "*Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.*"

Moja ya kazi nyingi alizofanya Yesu ni kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna.

Luka 4:40.

*Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake, akaweka mikono yake juu ya kila mmoja akawaponya.*

Yohana 10:10, "*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*"

Shetani hajawahi kuwa na huruma na maisha yako, hivyo hupaswi kuwa na

huruma wala ustaarabu kuhusiana na afya yako unapopata magonjwa. Ni mpango wa Mungu upokee uponyaji.

Matendo 10:38, "*Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye*."

Magonjwa na maradhi ni uonevu wa Ibilisi na wala sio kazi au baraka njema kutoka kwenye kwenye mkono mwema wa Mungu. Mungu hawezi kukupa zawadi ya magonjwa. Kwamba Mungu anakupenda

sana kiasi cha kukupatia magonjwa kwenye mwili wako.

Ni mpaka pale utakapojua kuwa ni uonevu wa Ibilisi ndio utaanza kuyakataa. Afya njema na uponyaji ni sehemu ya udhihirisho wa upendo wa Mungu kwenye maisha yetu.

Nimekuonyesha mambo yote mawili; afya ni kuzuia magonjwa yasiingie mwilini mwako kwa namna ya kiungu wakati huo huo uponyaji ni kuyaondoa magonjwa yaliyoingia mwili mwako kwa namna ya kiungu. Uko huru kuchagua afya au uponyaji wa kiungu!

Nimeshuhudiwa rohoni macho yako ndiyo yamefunguka kwa mshangao baada ya

kusoma sentensi hiyo juu… umeelewa sasa kuhusu afya ya kiungu… unachukua maamuzi ya kuwa na afya ili uwahudumie wenye magonjwa!

# NAMNA YA KUTEMBEA KWENYE AFYA YA KIUNGU.

Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kumsaidia mwamini kuhusiana na namna ya kutembea kwenye afya ya kiungu, na mojawapo ya mambo hayo ni;

1. **Tambua mapenzi ya Mungu kuhusiana na afya.**

Ni lazima ujue ni nini Mungu anasema kuhusiana na afya yako. Anayeamua hali (status) ya afya yako ni Mungu. Ni vizuri kuwasikiliza wataalamu wa afya (madaktari), wanasaikolojia, wataalamu wa *physiotherapy*, wabobevu kwenye maeneo

mbalimbali ya afya. Lakini hao wote sio waamuzi wa mwisho wa afya yako hivyo ni vizuri sana kuzingatia kile Mungu amesema kuhusu afya yako.

Kukosa neno linalohusiana na afya yako ni kujiweka kwenye hatari ya kupata mashambulizi ya magonjwa.
Swali la kukuongoza: Mungu anasemaje kuhusu afya yangu? Ni yapi mapenzi ya Mungu kuhusiana na afya yangu? Kwani, kuhusiana na afya ya kiungu kwangu neno la Mungu linasemaje?

Ukijiuliza maswali hayo kwa dhati ya moyo kama nilivyojiuliza mimi baada ya

kunusurika na hali ya umauti kutoka kwenye ugonjwa wa pumu (asthma). Haya maswali yatazalisha njaa ya kuyajua mapenzi ya Mungu kibinafsi na si kishabiki!

3 Yohana 1:1-2

*Mzee, kwa Gayo mpenzi, nimpendaye katika kweli. Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.*

- Ni mapenzi makamilifu ya Mungu ya kwamba wewe ufanikiwe katika mambo yote.
- Ni mapenzi makamilifu ya Mungu, wewe uwe na afya yako.

Kuwa na afya yako maana yake ni kuwa mbali na magonjwa, mbali na madhaifu, mbali na maumivu, mbali na mateso. Mungu anataka uwe mbali na haya yote kwa sababu hayatokani na Yeye.

2. **Aina hii ya afya yako inaamuliwa sana na hali ya roho yako**.

Hii afya inaanzia kwanza kwenye roho yako, ndani yako. Kule ndani ndio kutaamua hali ya afya yako ya nje iweje. Hali hii ya afya haitokei nje bali inatokea ndani kwenda nje (inside-out). Kwa hiyo hali yako ya ndani inaambukiza hali yako ya nje kiafya. Na hii huleta maaha halisi ya

afya ya kiungu kwa sababu inahusIsha afya ya roho yako na kuyagusa maeneno mengine yote ya nje ya mwili wako.

3. **Kwa sababu hiyo unahitaji kuilisha roho yako mlo kamili na kuifanyisha mazoezi.**

Kama afya hii inaanzia ndani basi ni lazima hiyo roho yako ipate aina sahihi ya chakula ili iweze kuzalisha afya nzuri kwenye mwili wako.

Wakolosai 3:16 *Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na*

*tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*

Hivyo haupaswi kupungukiwa wala kutindikiwa neno la Mungu hata kidogo. Na kama vile unavyoilisha roho yako ndivyo hivyo hivyo pia unavyopaswa kuifanyisha mazoezi.

1 Timotheo 4:8, "*Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote, yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye.*"

Kutokea kwenye mtindo huu wa uandishi wa usambamba (parallesim), mazoezi ya mwili yanafananishwa na utauwa (hali ya uungu ndani yako kama vile kumcha Mungu, kumpenda Mungu n.k). Yaani, kile mazoezi yanafanya kwenye mwili wako, ndicho utauwa hufanya kwenye utu wako wa ndani.

Hivyo ni lazima ujizoeze kuufanyia kazi utauwa; ukiroho wako, ili upate faida zinazombatana na kujizoeza huko, ambazo ni; Uzima/afya yako hapa duniani sasa.

Uzima kwenye maisha baada ya maisha ya duniani.

Kwa hiyo ukiilisha roho yako mlo kamili na ukiifanyisha roho yako mazoezi, basi utapata matokeo tarajiwa ya afya yako.

Huwezi kuwa umesoma kitabu hiki mpaka hapa na ukabaki mahali pamoja!
Afya iumbike na kuwa halisi ndani yako!

Kwa mamlaka ya neno la Mungu na jina la Yesu Kristo, magonjwa ya kurithi, ya kuambukizwa, ya umri, ya majira… yakuachie kwa jina la Yesu Kristo!

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**
Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764

jameskalekwa.com